# Simba 'kuwajua wabaya wao'



fikrapevu @fikrapevu @fikrapevu

# BUSATI

Ukweli na Uhakika

Tovuti: www.busati.co.tz | ISSN 3456-3421 Toleo Na.16 Busati Alhamisi Februari 6, 2025 Bei Tsh. 1,000 | Ksh. 100

## RAIS SAMIA AHAKIKISHIWA...

# Mitano tena inakuhusu

- DODOMA YAITIKA, WATANZANIA WAJITOKEZA KWA WINGI JAMHURI KUMPA HAKIKISHO HILO MAMA
- AWATAKA WATANZANIA KUIAMINI NA KUICHAGUA CCM KULETA UMOJA WA KITAIFA
- DK. MWINYI ANG'ARA, NAYE APEWA UHAKIKA WA MITANO TENA NDANI YA ZANZIBAR
- CCM YASEMA YATAKA UCHAGUZI WA UADILIFU



"Mkutano mkuu umesisitiza kwamba tunataka uchaguzi wa uadilifu, na kwakweli tungependa wana-CCM wote watuelewe tukisema uadilifu, mwenyekiti anamaanisha, kamati kuu inamaanisha na halmashauri kuu inamaanisha. Tunataka chama kisafi ambacho kiko tayari kutumikia wananchi"



## HISTORIA YA KUSISIMUA YA MJI MKONGWE KILWA

Utalii wa mambo ya kale na mambo ya kitamaduni ni sehemu kubwa sana ya utalii hapa Tanzania...

# Unapiga tambiko unataka nini?

# Rais Samia; Mitano tena inakuhusu

NA MWANDISHI WETU, Dodoma

**MITANO inakuhusu! Ndivyo Dodoma ilivyoitika jana wakati wa maadhimisho ya Miaka 48 ya kuasisiwa kwa Chama Cha Mapinduzi ambapo ilifanya sherehe zake jijini humo, ndani ya Uwanja wa Jamhuri.**

Itoshe tu kusema uwanja huo ulitapika, kwani ukiwa na uwezo wa kuchukua watu 20,000 idadi ilionekana kubwa zaidi na kuifanya sherehe hizo kunoga kwa kiasi kikubwa.

Mitano tena inakuhusu, ilikuwa salamu mahususi kwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan ambaye katika Uchaguzi Mkuu wa mwaka huu atasimama kuipeperusha bendera ya CCM na kupewa hakikisho hilo la kuchaguliwa kwa kishindo.

Hali ilikuwa ya shangwe wakati msafara wa Dkt. Samia ulipoingia uwanjani hapo ukiwa katika gari la wazi, huku akiwapungia maelfu ya watu waliojitokeza ambao walikuwa na shauku kubwa ya kumuona.

Hata wakati wa maandamano rasmi yaliyopita mbele yake, hali ya mambo ilikuwa shangwe, huku makundi ya sekta mbalimbali yakipita hapo, huku yakiimba nyimbo za kumsifu na kuimba kwa shangwe 'Mitano Tena'.

Baada ya hotuba yake iliyotanguliwa na ya mgombea wake mwenza, Dk. Emmanuel Nchimbi na ya Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dkt. Hussein Mwinyi, Dkt. Samia alishuka pamoja na viongozi hao na kuzunguka uwanja mzima wakiwa katika gari la wazi la CCM.

Katika hotuba yake, Dkt. Samia aliwakumbusha Watanzania kuendelea kuichagua CCM kutokana na kudumisha umoja wa kitaifa na kupigania maendeleo ya nchi hii.

"..Pia nataka niwakumbushe wana CCM kutobweteka, kwani mwaka huu tunataka kuzima zote na kuwasha ya kijani, tunapaswa kukipigania chama chetu," alisema, huku akiahidi kuiboresha UVCCM kwani ndiyo inayopika viongozi wa kitaifa.

Naye Katibu Mkuu wa Chama cha Mapinduzi (CCM), Dkt. Emmanuel Nchimbi, amesema chama hicho, kimedhamiria kuwa uchaguzi ujao utakuwa ni wa uadilifu na kwamba wanataka chama kisafi ambacho kitakuwa tayari kuwatumikia wananchi.

Dkt. Nchimbi amesema hayo jana katika kilele cha maadhimisho ya miaka 48 ya CCM yaliyofanyika katika Uwanja wa Jamhuri jijini Dodoma yenye kaulimbiu yake isemayo 'Shiriki uchaguzi kwa uadilifu, na kazi iendelee'

"Mkutano mkuu umesisitiza kwamba tunataka uchaguzi wa uadilifu, na kwakweli tungependa wana-CCM wote watuelewe tukisema uadilifu, mwenyekiti anamaanisha, kamati kuu inamaanisha na halmashauri kuu inamaanisha. Tunataka chama kisafi ambacho kiko tayari kutumikia wananchi"

Aidha, Dk John Nchimbi amesema sherehe hii imefanyika mwaka huu badala ya mwaka 2027, kufuatia maombi kutoka mikoa mbalimbali iliyotambua mafanikio makubwa ya Serikali chini ya chama hicho.

Aidha, Makamu Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Zanzibar na Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Mwinyi, amewataka wana-CCM kuhakikisha chama hicho kinaendelea kushika dola katika pande zote mbili za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kama inavyoelezwa katika Katiba ya CCM.

Dk. Mwinyi aliyasema hayo jana wakati wa kilele cha Maadhimisho ya Miaka 48 ya CCM, yaliyofanyika katika Uwanja wa Jamhuri, jijini Dodoma. Alipongeza viongozi, wanachama, na wapenzi wa CCM kwa mafanikio makubwa yaliyojiri katika kipindi hicho cha miaka 48.

"Kwa hakika, wana-CCM tunayo kila sababu ya kufurahi na kujivunia mafanikio makubwa ambayo chama chetu kimeyapata. Sote tunawajibika kuyadumisha mafanikio haya kwa kuimarisha umoja na mshikamano. Tunakabiliwa na uchaguzi mkuu mwishoni mwa mwaka huu, hivyo ni jukumu letu kuhakikisha chama chetu kinaendelea kushika dola," alisema Dk. Mwinyi.

Aidha, Dk. Mwinyi alisisitiza umuhimu wa kuwaandikisha wanachama wote katika daftari la wapiga kura na kuwahamasisha kwenda kupiga kura wakati wa uchaguzi, ili kuhakikisha CCM inashinda na kuendelea kushika dola.





# Ardhi wapongezwa kwa maktaba

NA MWANDISHI WETU

**KAMATI ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii imeipongeza Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa kutenga fedha kiasi cha Shilingi milioni 500 kwa ajili ya kukamilisha ujenzi wa maktaba ya Chuo cha Ardhi Tabora.**

Akizungumza hivi karibuni, katika kikao cha Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii wakati wa kupokea na kujadili taarifa ya utekelezaji Bajeti ya vyuo vya Ardhi Tabora (ARITA) na Morogoro (ARIMO) ya mwaka 2024/2025, Mwenyekiti wa Kamati hiyo Timotheo Mzava amesema, uamuzi wa Wizara kutenga fedha ni mzuri na muhimu katika maendeleo ya vyuo hivyo na wanafunzi kwa ujumla.

Msisitizo wa kamati yetu, vyuo hivi vya ardhi ni taasisi muhimu ya kuandaa wataalamu sambamba na kusaidia kazi, hivyo Wizara ya Ardhi iendelee kutupia jicho kwenye vyuo hivi ili vienedelee kufanya kazi yao inavyopaswa" amesema Mhe. Mzava.

Akizungumza wakati wa kuwasilisha taarifa za vyuo hivyo kwenye Kamati, Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi Deogratius Ndejembi aamesema Wizara yake imepokea maelekezo ya kamati kwa utekelezaji na ufanisi wa vyuo hivyo.

Kikao hicho cha Kamati ya Bunge kimehudhuriwa Viongozi wa Wizara akiwemo Katibu Mkuu Mhandisi Anthony Sanga, Naibu Katibu Mkuu Lucy Kabyemela, Wajumbe wa Menejimenti ya wizara pamoja na watendaji wa vyuo vya ARITA na ARIMO.

# Watakiwa kutatua kero za wananchi

NA ALBANO MIDELO, Songea

**KATIBU Tawala wa Mkoa wa Ruvuma Mary Makondo ameziagiza Halmashauri zote nane kushughulikia kero na malalamiko ya wananchi kwa ufanisi zaidi.**

Agizo hilo limetolewa katika Baraza la Madiwani la Halmashauri ya Wilaya ya Songea, lililofanyika katika Ukumbi wa Halmashauri Lindusi. Katika kikao hicho, Katibu Tawala wa Mkoa wa Ruvuma aliwakilishwa na Amina Tindwa.

Katika hotuba yake, Tindwa alisisitiza kuwa taasisi zote za umma zinapaswa kushughulikia malalamiko ya wananchi kwa mujibu wa maelekezo kutoka TAMISEMI na Ofisi ya Rais – Menejimenti ya Utumishi wa Umma.

Alisema kuwa hatua hii ni sehemu ya utekelezaji wa Ilani ya Chama cha Mapinduzi na kuimarisha uwajibikaji wa watumishi wa umma.

Aidha, Tindwa ameagiza kuanzishwa kwa ofisi maalum za malalamiko katika halmashauri zote, ili kusaidia Serikali kusikiliza na kutatua kero za wananchi waliowachagua viongozi wa umma.

Amelitaja lengo la kushughulikia kero za wananchi ni kupunguza manung'uniko na kuhakikisha kuwa serikali inatekeleza majukumu yake kwa ufanisi na uwajibikaji.

# TASAF yaendelea kupewa fedha

NA MWANDISHI WETU

**SERIKALI ya Awamu ya Sita, kwa kushirikiana na wadau mbalimbali, inaendelea kutoa fedha kwa ajili ya Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF).**

Mkuu wa Wilaya ya Songea, Kapenjama Ndile,akifungua kikao cha tathmini ya mpango wa kunusuru kaya maskini (TASAF) kwa wataalam wa ngazi ya Mkoa, Wilaya, na Halmashauri, kilichofanyika katika ukumbi wa Heritage Cottage mjini Songea, amesema Mkoa wa Ruvuma umepokea zaidi ya shilingi bilioni 12 kwa mwaka 2024 kwa ajili ya TASAF

Akizungumza kwa niaba ya Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma, Ndile alieleza kuwa fedha hizo zinalenga kusaidia kaya maskini kuongeza kipato, kupata fursa za kiuchumi, na kuboresha maisha yao kupitia uwekezaji kwa watoto ili kuhakikisha wanapata elimu na maarifa ya kujikwamua kiuchumi.

Amesisitiza umuhimu wa kuzingatia miongozo ya serikali ili kuhakikisha fedha hizo zinasimamiwa ipasavyo na kuleta matokeo chanya kwa wananchi.

Naye Mratibu wa TASAF Mkoa wa Ruvuma, Xsaveria Mlimira, alifafanua kuwa kati ya Januari na Desemba 2024, kaya 47,721 zimeendelea kunufaika na mpango huo, huku kaya 18,912 zikiwa zimehitimu.

Amesema Mpango huo sasa uko katika awamu ya pili ya utekelezaji na unahusisha vijiji na mitaa 85 kutoka Wilaya zote za mkoa.

Kwa upande wa wanufaika, Regina Komba ameushukuru mpango wa TASAF kwa kumwezesha kuwasomesha watoto wake, jambo ambalo asingeliweza kufanya bila msaada huo.

Suzan Komba, mnufaika mwingine, alisema kupitia mpango huo ameweza kuanzisha miradi ya ufugaji wa kuku na nyuki, ambayo imemsaidia kuendesha maisha yake kwa uhakika

# Unapiga tambiko unataka nini?

NA MWANDISHI WETU

**TAMBIKO ni desturi za kimila au kidini zinazofanywa na watu wa jamii mbalimbali kwa madhumuni ya kiroho, utamaduni au kuenzi mababu.**



Hata hivyo, tambiko zinaweza kuwa na madhara na athari zisizofaa kwa watu binafsi, familia na jamii kwa ujumla. Katika makala hii, tutajadili hasara na madhara ya tambiko kwa kina.

**1. Kuleta Imani Potofu**

Kushawishiwa na Usadikisho wa Kisiasa au Kihisia: Tambiko mara nyingi hutegemea imani za kimila au za kiroho ambazo si kila wakati zina msingi wa kisayansi.

Watu wanaoweza kudhani kuwa tambiko linaweza kutatua matatizo yote wanaweza kupoteza uwezo wa kutafuta suluhisho la kiuhalisia au kiakili, na hivyo kuchangia matatizo yasiyo na msingi.

Kuongeza Woga na Wasiwasi: Tambiko mara nyingi huchochea woga na wasiwasi, hasa pale ambapo limejengwa katika imani ya kwamba mababu au miungu inaweza kuwaadhibu wale wasiofanya tambiko.

Wasiwasi huu unaweza kuwa mzigo wa kihisia kwa mtu binafsi, ambao unaweza kuathiri afya ya akili na ustawi wa mtu.

**2. Gharama Kubwa**

Matumizi ya Rasilimali: Tambiko mara nyingi yanahitaji matumizi ya pesa nyingi kwa ajili ya kununua vifaa maalum, wanyama wa sadaka, na gharama za kuhudumia wageni.

Hii inaweza kuathiri kifedha familia au mtu binafsi, hasa wale ambao kipato chao ni kidogo.

Badala ya kutumia pesa kwa mambo muhimu kama elimu, afya, au maendeleo ya kiuchumi, rasilimali hutumika kwa tambiko, na hivyo kudumaza maendeleo ya kifamilia na ya kiuchumi.

**3. Madhara ya Kiafya na Kijamii**

Kutumia Vinywaji au Madawa Yanayodhuru: Baadhi ya tambiko yanahusisha matumizi ya vinywaji au madawa ambayo yanaweza kuwa na madhara kwa afya.

Wakati mwingine, watu hulazimika kunywa dawa za kienyeji ambazo hazijathibitishwa kiafya, jambo ambalo linaweza kusababisha madhara kama sumu au magonjwa yasiyo ya lazima.

Kuchochea Ubaguzi na Kutengana kwa Jamii: Wakati mwingine, tambiko huweza kuchochea migawanyiko katika jamii.

Wale ambao hawashiriki au hawafuati tambiko fulani wanaweza kujikuta wakitengwa au kubaguliwa na jamii yao. Hii inaweza kuleta chuki, migogoro, na kuhatarisha mshikamano wa kijamii.

**4. Kuzuia Maendeleo na Maarifa ya Kisasa**

Kukwamisha Teknolojia na Maarifa Mapya: Watu wanaoshikilia sana tambiko wanaweza kupuuza maendeleo ya kisayansi na maarifa ya kisasa.

Badala ya kutumia matibabu ya kisasa au mbinu bora za kilimo, watu wanaweza kushikilia imani za tambiko na hivyo kukwamisha maendeleo yao wenyewe na ya jamii.

Kuwazuia Watu Kutafuta Suluhisho Bora: Wakati watu wanapokuwa na shida au changamoto, wanaweza kuamini kuwa tambiko litawasaidia badala ya kutafuta msaada wa kitaalamu.

Kwa mfano badala ya kwenda hospitali kwa matibabu, mtu anaweza kufuata tambiko kwa imani kuwa litasaidia, na hivyo kuchelewesha au kukosa matibabu bora.

**5. Madhara ya Kimaadili**

Kutumia Sadaka ya Wanyama au Mali: Baadhi ya tambiko yanahusisha kutoa sadaka za wanyama, jambo ambalo linapingana na kanuni za haki za wanyama.

Aidha sadaka za mali zinaweza kuathiri familia, kwani mali inayotolewa kwa tambiko inaweza kuwa ya msingi kwa maisha ya kila siku ya familia.

Kusababisha Shinikizo la Kijamii: Mara nyingi, watu hulazimishwa kushiriki tambiko kutokana na shinikizo la kijamii.

Watu wanaweza kushiriki kwa kulazimishwa au kwa woga wa kukataliwa na jamii.

Hii inapingana na uhuru wa mtu binafsi na inaweza kuathiri faraja na amani ya mtu.

**6. Athari kwa Mazingira**

Uharibifu wa Mazingira: Tambiko zinazohusisha kuchinja wanyama kwa wingi, kukata miti kwa ajili ya kuni, au kutumia mazao maalum yanaweza kuathiri mazingira.



# Una roho ngumu? Jiajiri



NA MWANDISHI MAALUM

**KUJIAJIRI ni pale mtu anapoanzisha biashara au shughuli ya kiuchumi kwa kujitegemea badala ya kuwa mwajiriwa kwa mtu au kampuni.**

Ingawa kujiajiri kuna faida nyingi kama uhuru wa kiutendaji na fursa ya kuongeza kipato, kuna changamoto nyingi na madhara yanayoweza kusababisha matatizo ya kifedha, kisaikolojia, na hata kijamii.

Hapa chini tunajadili baadhi ya hasara na madhara ya kujiajiri.

**1. Kukosa Uhakika wa Kipato**

Wajasiriamali wanakosa kipato thabiti na mara nyingi kipato chao hutegemea mafanikio ya biashara, hivyo:

Kutokuwa na kipato cha uhakika; mara nyingi mapato yanaweza kubadilika kila mwezi, na baadhi ya miezi inaweza kuwa na kipato kidogo au hata kutokuwa na kipato kabisa.

Gharama za awali za kuanzisha biashara zinaweza kuwa kubwa, na wajasiriamali wanaweza kushindwa kupata kipato cha kutosha kufidia gharama hizo katika miezi ya kwanza.

**2. Muda Mrefu wa Kazi na Kazi Ngumu**

Wajasiriamali wengi hulazimika kufanya kazi kwa muda mrefu na kujituma zaidi ili biashara zao ziweze kustawi:

Upungufu wa muda wa kupumzika na kuwa na usawa kati ya kazi na maisha binafsi; mara nyingi kazi inaweza kuchukua muda mwingi, hivyo kuathiri muda wa familia na wa kijamii.

Kukabiliwa na kazi nyingi na ngumu, hasa mwanzoni, ambapo mmiliki anaweza kuwa ndiye mfanyakazi pekee anayesimamia kila kitu – kuanzia masuala ya fedha hadi masoko.

**3. Shinikizo la Kiuchumi na Hatari ya Kupata Hasara**

Biashara zinakabiliwa na hatari nyingi za kiuchumi ambazo zinaweza kusababisha madhara makubwa kifedha:

Hatari ya kupata hasara; kwa kuwa hakuna uhakika wa faida, mmiliki anaweza kuwekeza fedha nyingi bila kujua kama biashara itazalisha faida au la.

Shinikizo la kushindana na wafanyabiashara wengine, hasa kwenye sekta zenye ushindani mkubwa, linaweza kuongeza gharama za kuendesha biashara na kupunguza faida.

**4. Majukumu Mengi na Shinikizo Kubwa**

Kujiajiri kunakuja na majukumu mengi ambayo mmiliki anatakiwa kuyasimamia:

Kubeba mzigo wa maamuzi yote muhimu ya biashara, jambo ambalo linaweza kusababisha msongo wa mawazo, hasa wakati wa kufanya maamuzi ya kifedha na kimkakati.

Kuhitaji kuzingatia mambo mengi, kama vile kulipa kodi, kusimamia wafanyakazi (endapo anawaajiri), na kutunza mahusiano na wateja, mambo ambayo yanahitaji umakini na maarifa mengi.

**5. Matatizo ya Kisaikolojia na Msongo wa Mawazo**

Changamoto za kifedha, shinikizo la kazi, na majukumu mengi huweza kuleta madhara ya kisaikolojia kwa wajasiriamali:

Msongo wa mawazo na wasiwasi kuhusu hatma ya biashara; kwa kuwa hakuna uhakika wa mafanikio, mjasiriamali anaweza kuwa na wasiwasi mwingi kuhusu upotevu wa mtaji na madhara yanayoweza kujitokeza.

Hofu ya kushindwa au kukosa faida inayoendana na jitihada, hali inayoweza kumkatisha tamaa mjasiriamali na kudhoofisha jitihada zake.

**6. Kukosa Fursa za Mafao ya Ajira**

Wajasiriamali wanakosa baadhi ya faida za kisheria na kiuchumi zinazopatikana kwa waajiriwa, kama vile:

Mafao ya kustaafu, bima ya afya, na ruhusa za malipo, kwa kuwa mfanyabiashara ana jukumu la kuhakikisha anajiwekea akiba mwenyewe kwa ajili ya malipo hayo, jambo ambalo linaweza kuwa gumu katika mazingira ya biashara yenye kipato kisichotabirika.

# Umuhimu wa Kutunza Mazingira

NA MWANDISHI MAALUM

**KUTUNZA mazingira ni jukumu muhimu linalohitaji kushirikisha jamii nzima ili kufanikisha maendeleo endelevu na kulinda rasilimali kwa vizazi vya sasa na vijavyo.**



Mazingira yanajumuisha hewa, ardhi, maji, mimea, wanyama na viumbe hai wengine wanaoishi katika mfumo unaotegemeana.

Hapa tunachunguza kwa kina faida na umuhimu wa kutunza mazingira, jinsi inavyoweza kuboresha maisha yetu na kuendeleza uchumi na hatari zinazoweza kutokea tukiyapuuza.

**1. Faida za Kutunza Mazingira**

Afya Bora kwa Jamii: Mazingira safi yanaathiri moja kwa moja afya ya binadamu. Hewa safi, maji safi na chakula kisichochafuliwa na kemikali ni muhimu kwa afya njema.

Mazingira safi yanazuia magonjwa yanayoenezwa na uchafu kama vile malaria, kipindupindu na homa ya matumbo ambayo mara nyingi husababishwa na maji machafu na mazingira yasiyotunzwa.

Kupunguza Athari za Mabadiliko ya Tabianchi: Mazingira yanapokuwa safi na yanapotunzwa vyema, yanachangia kupunguza mabadiliko ya tabianchi.

Misitu huchukua na kuhifadhi dioksidi kaboni ($CO_2$), gesi inayochangia ongezeko la joto duniani.

Kwa kutunza misitu na kupunguza uchomaji wa kuni na mkaa, tunaweza kupunguza athari za mabadiliko ya tabianchi ambayo huleta ukame, mafuriko na majanga mengine ya asili.

Kuboresha Ustawi wa Kiuchumi: Mazingira safi na yenye rutuba yanachangia kwenye ukuaji wa uchumi.

Kilimo, ufugaji na uvuvi hutegemea mazingira yenye afya ili kuwa na mavuno bora na bidhaa za kutosha kwa soko.

Pia utalii wa mazingira kama vile utalii wa wanyamapori na vivutio vya asili, unachangia pato la taifa na ajira hasa katika nchi zinazoendeleza sekta ya utalii.

Kuhifadhi Viumbe Hai: Mazingira safi na yasiyochafuliwa husaidia kuhifadhi viumbe hai ambao ni sehemu muhimu ya mnyororo wa chakula na usawa wa ikolojia.

Kila kiumbe, kuanzia mdogo kama bakteria hadi mkubwa kama simba, kina nafasi maalum katika ikolojia.

Kwa kutunza mazingira tunahakikisha kwamba viumbe hawa wanaendelea kuishi na kudumisha mifumo muhimu ya mazingira inayowezesha maisha.

Kuwezesha Upatikanaji wa Maji Safi: Kwa kutunza vyanzo vya maji kama mito, maziwa, na chemchemi, tunaweza kuhakikisha upatikanaji wa maji safi kwa matumizi ya binadamu na wanyama.

Uchafuzi wa maji unaotokana na plastiki, kemikali na mafuta unaweza kuepukwa kwa juhudi za kutunza mazingira.

Hii ni muhimu kwani maji ni uhai na ni msingi wa ustawi wa viumbe hai wote.

**2. Umuhimu wa Kutunza Mazingira**

Kuendeleza Maisha ya Vizazi Vijavyo: Kutunza mazingira ni njia ya kuhakikisha kuwa vizazi vijavyo vinaweza kufurahia rasilimali za asili na kuwa na mazingira bora ya kuishi.

Ikiwa tutaendelea kuchafua na kuharibu rasilimali zetu bila mpango, vizazi vijavyo vitakosa ardhi ya kilimo, maji safi na hewa safi na hivyo kupata changamoto kubwa za kiuchumi na kijamii.

Kudumisha Usawa wa Kiasili (Ikolojia): Mazingira yanatengeneza mfumo wa kiikolojia ambapo viumbe hai hutegemeana.

Mimea hutegemea wadudu kwa uchavushaji, wakati wanyama hutegemea mimea kwa chakula na malazi.

Kuwapo kwa usawa wa viumbe hawa ni muhimu kwa ustawi wa mazingira na usawa huu unaweza kuvurugwa ikiwa mazingira hayatatunzwa ipasavyo.

Kuzuia Majanga ya Asili: Mazao ya asili kama miti na mimea mingine husaidia kuzuia mmomonyoko wa ardhi, mafuriko, na maporomoko ya udongo.

Kwa kulinda mazingira kwa kupanda miti na kuhifadhi maeneo ya asili, tunapunguza hatari ya majanga haya ambayo yanaweza kusababisha vifo, uharibifu wa mali na matatizo ya kiuchumi.

Kuboresha Ufanisi wa Kilimo na Usalama wa Chakula: Kilimo kinaathiriwa sana na hali ya hewa, ardhi na vyanzo vya maji.



# Pale unapohitaji kufungua kampuni yako

NA MWANDISHI WETU

**UNAPASWA kujua vitu vya kuzingatia Kabla ya kufungua kampuni au kufungua biashara yako Tanzania ili uweze kupata mafanikio katika siku za mbeleni kwenye maisha yako.**




**1. Chagua wazo bora la biashara**

Katika eneo ambalo watu wengi hukosea wakati wanapoanzisha kampuni au biashara ni uchaguzi wa wazo la kibiashara.

Unapochagua wazo baya au usilolimudu, ni wazi kuwa hutoweza kulitekeleza na kupata faida. Hakikisha wazo unalolichagua unalimudu vyema pia linatekelezeka.

Epuka kuchagua wazo pana sana au kuchagua wazo kwa sababu mwingine analifanya. Kwa kuwa wewe unaanza ni vyema ukachagua wazo unalolipenda, kulimudu vyema na linaloweza kukupa faida.

**2. Fanya utafiti wa biashara**

Kabla ya kuacha kazi yako au kile unachokifanya ili uanzishe kampuni yako, ni vyema ukafanya utafiti wa kina juu ya biashara utakayofanya.

Mambo ya kufanyia utafiti ni: Elewa biashara yako na huduma utakayotoa. Fahamu wateja wako. Fahamu ushindani. Wafahamu watu utakaofanya nao kazi. Fahamu njia bora ya mauzo ya bidhaa au huduma yako

**3. Andaa 'business plan'**

Baada ya kufanya utafiti, sasa weka wazo au mpango wako katika karatasi. Mpango huu utakuwezesha kukuongoza katika kufikia malengo yako.

Kimsingi mpango wako wa biashara utajumuisha mambo kama vile: Mwonekano wa jumla wa kampuni. Muundo wa utawala. Ufafanuzi/ Maelezo ya kampuni. Malengo, Maono na mikakati. Maelezo juu ya soko na tasnia unayoingia kufanya biashara

Uendeshaji. Mpango wa matumizi ya fedha. Pamoja na taarifa nyingine za msingi zinazohusiana.

**4. Bainisha chanzo cha fedha**

Ni lazima kubaini chanzo cha fedha utakazozitumia kuanzisha biashara au kampuni yako. Je fedha hizo zitatokana na mkopo, akiba yako au msaada?

Kumbuka uendeshaji wa kampuni unahitaji fedha kwa ajili ya shughuli mbalimbali kama vile matumizi ya ofisi, usafiri, malipo ya huduma na mishahara.

Ni vyema kulishughulikia hili mapema ili usije ukakwama katika biashara yako.

**5. Tambua muundo wa biashara**

Unatakiwa kubainisha muundo wa biashara au kampuni yako kabla hujaianzisha. Je kampuni au biashara yako itakuwa ni ya shirika, ubia au binafsi?

Unapochagua muundo zingatia yafuatayo: Ugumu wa uendeshaji kwa kila mfumo. Gharama za uendeshaji. Kodi. Sheria na vibali. Manufaa ya muundo husika. Mtaji. Unapozingatia haya hakika utaweza kuchagua muundo wa kampuni au biashara wenye tija zaidi kwako.

**6. Tafuta ofisi ya biashara**

Watu wengi wamekuwa wakianzisha kampuni kwa mazoea bila kuzingatia kuwa ofisi ni muhimu kwa biashara au kampuni zao.

Tafuta ofisi utakayo mudu gharama zake, pia yenye kukidhi mahitaji ya kampuni au biashara yako.

Kama utaamua kufanyia kazi nyumbani, basi hakikisha unatenganisha mambo binafsi na yale ya ofisini. Kumbuka kuepuka kuchagua ofisi ya kifahari au ya gharama kubwa bila sababu ya msingi.

**7. Changanua changamoto za biashara**

Changamoto zipo kila mahali hivyo yakupasa kuzifikiria kabla ya kuanza kampuni au biashara yako. Kama unajidanganya kuwa utafanya biashara bila kukutana na changamoto yoyote unajidanganya.

Jitahidi uzitambue changamoto mapema ili uweze kuweka mikakati mapema ya namna utakavyo pambana nazo.



# Afrika lazima ipambane yenyewe kujiokoa na maagizo ya Trump

**HATUA ya Rais wa Marekani Donald Trump kusaini agizo la kuiondoa nchi hiyo katika Shirika la Afya Duniani (WHO) siku chache zilizopita imeanza kuleta athari kadhaa hususan barani Afrika kama ilivyotarajiwa.**

Licha ya kuwa kuna sheria zinazohitajika kufuatwa kwa taifa linalotaka kundoa ufadhili wake, utawala wa kiongozi huyo mpya tayari umechukua hatua ya kusitisha usambazaji wa dawa za kuokoa maisha za HIV, malaria na kifua kikuu mbali na dawa za watoto wachanga katika mataifa yote yanayosaidiwa na shirika la USAID duniani.

Athari hizo zinatokana na Marekani kuwa mchangiaji mkubwa wa kifedha wa WHO na programu mbali mbali zilizopo chini ya shirika hilo na taasisi nyingine kubwa za kiafya duniani.

Siku ya Jumanne, wakandarasi na washirika wanaofanya kazi na Shirika la Misaada la Marekani (USAID) nchini Tanzania na Kenya walianza kupokea barua hizo ili kusitisha ufadhili huo mara moja, kulingana na vyanzo.

Hatua hiyo ni sehemu ya kusitishwa kwa misaada kwa Marekani na ufadhili uliowekwa tangu Trump aingie madarakani Januari 20, huku programu zikikaguliwa.

Afisa Mkuu wa Kituo cha Kudhibti Magonjwa barani Africa (CDC) Ngashi Ng'ongo amenukuliwa akisema nchi nyingi zimekuwa zikitegemea uwekezaji wa Marekani kupitia WHO kufadhili shughuli za afya ya umma.

"Tunajua jukumu ambalo WHO imecheza katika bara... kuboresha utoaji wa programu za afya," Ng'ongo aliambia mkutano na wanahabari.

"Kupunguzwa au kukatwa kwa ufadhili wa (Marekani) bila shaka kutaathiri mwitikio. Ni wakati kwa baadhi ya nchi wanachama wa Afrika kufikiria upya ufadhili wa afya ya umma," alisema.

Nchini Kenya na Tanzania tayari Shirika la Misaada ya Kimataifa la Marakani (USAID) limetangaza kupunguza au kufuta shughuli kadhaa katika programu zake.

Katika taarifa zilizotumwa na USAID, Shirika hilo lilisema kuwa linakatiza huduma zote zilizokuwa zikitolewa na USAID kufuatia agizo la Rais Trump la kuiondoa nchi hiyo katika WHO.

USAID imeyataka mashirika yanayopokea ufadhili huo kufuata agizo hilo ili kuhakikisha kwamba hayagharamiki na huduma zozote zilizokatizwa.

Tayari WHO limeelezea wasiwasi wake kuhusu athari za kusitishwa kwa ufadhili wa mara moja wa programu za VVU katika nchi za kipato cha chini na cha kati.

Kupitia taarifa iliYotumwa katika vyombo vya habari, shirika hilo limesema kwamba kusitishwa kwa ufadhili wa programu za VVU kunaweza kuwaweka watu wanaoishi na VVU katika hatari ya mara moja ya magonjwa, kifo na kudhoofisha juhudi za kuzuia maambukizi katika jamii na nchi.

WHO imesema kwamba hatua kama hizo, zikiendelea, zinaweza kusababisha kuongezeka kwa maambukizi mapya na vifo, kurudisha nyuma miongo kadhaa ya maendeleo na uwezekano wa kurudisha ulimwengu kwenye miaka ya 1980 na 1990 wakati mamilioni ya watu walikufa kwa VVU kila mwaka duniani.

Kwa mujibu wa Daktari Allen Malache wa Shirika la Kelan nchini Kenya, athari miongoni mwa wahudumu wa afya zitashuhudiwa iwapo agizo hilo la Trump litaendelea kwa takriban miezi mitatu.

"Iwapo hakutapatikana huduma za Kiafya kwa wale wanaozihitaji hususan katika kliniki zinazosimamiwa na mashirika kama vile Pepfar, wale wanaotoa huduma hizo watafanya kazi gani?

"Wale wanaopokea huduma wataenda kupata huduma upande gani iwapo kiliniki zinazosimamiwa na fedha zinazotoka kwa Pepfar zitakuwa zimefungwa. Kwa mfano vituo vinavyosimamia Ukatili wa Kijinsia vikifungwa watu watapata shida kwasababu watu watahitaji kupata ushauri nasaha na matibabu."

Aliongezea kusema kwamba ni muhimu Wamarekani kutathmini upya uamuzi huo ili kuona jinsi watu watakavyotatizika kutokana na hatua hiyo.

Dk. Lawi Mwenda amesema madhara makubwa yatapatikana katika huduma kama vile za Malaria, Kifua Kikuu na HIV ambapo wagonjwa wengi wanatumia dawa za maradhi hayo.

Dkt. Lawi vilevile ameongezea kuwa changamoto itakuwa katika utafiti wa dawa mpya na hela ambayo inatumika katika mikakati ya kuzuia maambukizi mapya

Afrika inaweza kujisimamia yenyewe?

Kwa mujibu wa Daktari Lawi Mwenda, hela nyingi zinazotolewa na mashirika ya misaada ya kiafya kama vile USAID na Global Fund ni hela ambazo asilimia kubwa zinatumika kwa utafiti.

"Hizi dawa mpya ndizo zinazokula hela nyingi zaidi kuliko dawa zinazogawanywa hospitalini. Baadhi ya tafiti zinazofanywa hata Wamarekani wanazihitaji."

Daktari huyo anasema kwamba wizara nyingi zinazosimamia afya barani Afrika hazitaathirika pakubwa kwa kuwa kuna dawa nyingi na kwamba mataifa mengi ya Afrika yana uwezo wa kuzalisha dawa hizo barani na kugharamikia ARVs.

Alisema: "Kuna nchi nyingi zinazoweza kutengeneza dawa kama vile Afrika Kusini ambayo ina uwezo wa kuzalisha dawa za ARVs, Uganda kuna kampuni ya Shippler, Kenya kuna Universal Cooperation Limited, Zambia, Ethiopia na hata Tanzania kuna viwanda vilivyo na uwezo wa kuzalisha dawa."

Amesema kwamba licha ya kuwa kuna dawa zinazotoka India zinatozotumiwa na baadhi ya wagonjwa kuna aina hiyohiyo ya dawa zinazozalishwa Afrika.

"Marekani wanaweza kuwa wamesitisha lakini sio wao ambao wanazalisha au kufadhili asilimia 100, baadhi ya serikali za Afrika zinagharamia dawa hizi asilimia 20 na nyengine asilimia 40, kwa hivyo ninaamini kwamba serikali zetu za Afrika zina uwezo wa kugharamia."

Amesema kwamba gharama ambazo zinatokana na dawa za HIV ni gharama ambazo serikali nyingi barani Afrika zinaweza kumudu.

Hatahivyo Dkt. Allen anasema kwamba ni wakati ambapo mataifa ya Afrika yanapaswa kujiuliza iwapo yanaweza kugharamikia huduma hizi kupitia utengaji wa fedha au zitaendelea kufanya mambo mengine yasio na muhimu mkubwa wa Kiafya?

"Serikali zetu zimejikokota sana ili kufikia kiwango ambacho zinaweza kusimamia matibabu. Kenya tuna katiba inayosema kwamba serikali ina jukumu la kuhakikisha kuwa kila Mkenya anapata haki yake ya Afya. Kutokana na sheria hiyo basi jukumu ni sio la Uingereza au Marekani, jukumu ni letu sisi wenyewe," alihitimisha.

# Kudai hujui utamaduni wako ni kujiuza mwenyewe

NA MWANDISHI WETU

**UTAMADUNI ni mfumo wa maisha unaojumuisha imani, mila, desturi na maadili yanayoongoza maisha ya jamii fulani. Ni urithi wa kipekee unaotambulisha watu na kuwapa utambulisho wa asili.**



Katika jamii yoyote, utamaduni ni kiini muhimu kwa maisha ya kila siku na umeendelea kuwa na mchango mkubwa katika kuleta mshikamano na ustawi wa watu.

Hapa tunachambua faida na umuhimu wa utamaduni katika kuimarisha maisha na maendeleo ya kijamii, kiuchumi na kisaikolojia.

**1. Utambulisho wa Jamii**

Utamaduni unawapa watu utambulisho wa kipekee. Mila na desturi zinazohusiana na mavazi, lugha, chakula, na shughuli za kila siku huwa ni alama zinazowatofautisha watu wa jamii moja na nyingine.

Kwa mfano, mavazi ya kimila kama vile vitenge na kanga katika Afrika Mashariki ni sehemu ya utambulisho wa watu wa maeneo hayo.

Kwa kuwa na utamaduni wao, jamii hujihisi huru na wenye kujiamini, na hivyo kuimarisha mshikamano wao wa kijamii.

**2. Kujenga Mshikamano na Umoja**

Utamaduni unaunganisha watu kwa njia maalum. Sherehe, tamaduni za kimila, na ibada za kidini huwaleta watu pamoja kwa matukio muhimu kama harusi, sherehe za kuzaliwa, na mazishi.

Hii inajenga mshikamano na undugu baina ya watu, kwani wanajifunza kushiriki na kusaidiana katika nyakati zote.

Ushiriki wa pamoja katika shughuli za kitamaduni unaleta umoja na kuimarisha uhusiano wa kifamilia na kijamii.

**3. Kukuza Maadili na Nidhamu**

Utamaduni una athari kubwa katika kujenga maadili na nidhamu ya jamii. Mila na desturi huweka kanuni zinazowaongoza watu katika tabia zao za kila siku.

Kwa mfano, utamaduni wa kuwasalimu wakubwa, kuheshimu wazazi, na kusaidiana, unaimarisha nidhamu na unyenyekevu. Vilevile jamii huweza kujifunza kuishi kwa kuheshimu mipaka na sheria, ambayo inasaidia kupunguza migogoro na kujenga jamii yenye amani.

**4. Uhifadhi wa Maarifa na Urithi**

Utamaduni unachangia kuhifadhi historia na maarifa ya jamii kutoka kizazi kimoja hadi kingine.

Nyimbo za kitamaduni, hadithi, na methali ni njia muhimu zinazotumika kuwasilisha hekima ya zamani kwa vijana wa sasa.

Maarifa haya yanajumuisha taarifa kuhusu mimea tiba, mbinu za kilimo, na njia za kuishi katika mazingira ya asili.

Kwa kupitia tamaduni hizi, maarifa na hekima ya kale huendelea kuishi katika vizazi vijavyo.

**5. Maendeleo ya Sanaa na Ubunifu**

Utamaduni unahamasisha ubunifu na maendeleo ya sanaa. Miondoko ya ngoma, muziki, na michoro hutokana na mila na desturi za kitamaduni, ambayo inachangia maendeleo ya vipaji na kuongeza thamani ya jamii katika ulimwengu wa sanaa.

Wasanii na wabunifu wa kazi za mikono wanatumia maarifa ya kitamaduni kubuni bidhaa kama vile vikapu, mapambo, na vinyago ambavyo vina thamani kiutamaduni na kiuchumi.

**6. Kuimarisha Utalii na Uchumi**

Utamaduni una mchango mkubwa katika sekta ya utalii, ambayo huleta pato kwa nchi na jamii.



# Historia ya kusisimua ya Mji Mkongwe Kilwa

NA MWANDISHI WETU

**TANZANIA ni nchi iliyo barikiwa sana na uwepo wa vivutio vingi vya kila aina, kuna vivutio vya wanyama, misitu, milima, mambo ya kale, utamaduni na fukwe za bahari. Hivyo karibu kila sehemu ya Tanzania ina vivutio vya utalii.**

Kati ya vivutio vyote hivyo, vivutio vya wanyamapori ndio hujulikana zaidi na watu wengi kuliko vivutio vyote. Kwa kiasi kikubwa vivutio vya wanyamapori vimekuwa vikitangazwa kila mara na watu wengi wanafahamu kuwa wanyamapori ni vivutio na wanahamasika kutembelea mbuga za wanyama kwa ajili ya kujionea vivutio hivyo.

Kwa kuwa tuna utajiri wa vivutio vingi namna haii, sekta ya utalii haina budi kuwa na mikakati ya muda mrefu ya kuhakikisha kila sehemu yenye vivutio inatangazwa na kujulikana kitaifa na kimataifa.

Utalii wa mambo ya kale na mambo ya kitamaduni ni sehemu kubwa sana ya utalii hapa Tanzania, tuna kila kinachofaa kutufanya kuwa mstari wa mbele kwenye masuala ya utalii.

Kwenye makala hii nitazungumzia kuhusu utalii wa mambo ya kale, mambo ya kale au historia za mabo ya kale ni sehemu ambayo inakuwa na mvuto kitaifa na kimataia endapo itapewa kipaumbele na kutangazwa ipasavyo na vyombo husika.

Tanzania ina historia ndefu sana ya mambo ya kale, kuna historia ambazo zimekuwapo tangu karne ya 9, sehemu zenye historia hizi ni sehemu za ajabu sana na zina hadithi za kusisimua kuhusu maisha ya watu waliowahi kuishi sehemu hizi ambazo zina mabaki na historia hii.

Mji wa Kilwa, ni miongoni mwa miji ya ajabu sana katika historia ya maisha ya binadamu, kuna historia ya kusisimua sana kweye miji hii, mji wa Kilwa ni kati ya miji mikongwe sana hapa dunini. Ni mji ambao ulipata mafanikio na kuwa maarufu kutokana na kumiliki biashara ya dhahabu.




Mji huu unafahamika kama kitovu cha biashara katika karne ya 9 hadi 15, na 16. Kabla ya ukoloni kuingia biashara kubwa ilikuwa ni dhahabu. Hivyo kwa kuwa mwenye dhahabu ndie mwenye nguvu basi, mji huu wa Kilwa uliendelea kushika hatamu kwa kipindi kirefu sana kutawala sehemu kubwa hadi sehemu za kusini karibia na Zimbabwe.

Kwa kuwa mji huu ulijulikana kama kitovu cha biashara kwa muda mrefu katika pwani ya Afrika Mashariki, kuna maeneo ya mji huu yalijengwa vizuri sana, maeneo hayo yalijengwa na mabaki yake yanaweza kuonekana hadi leo. Meneo ya Kilwa Kisiwani ndio yalikuwa ni kitovu na sehemu kuu ya biashara hii, ambayo hujulikana kama mji wa masultani.

Kukua na kuwa na nguvu kwa mji huu wa Kilwa Kisiwani haukwenda mbali sana, historia inaonyesha katika karne ya 15 mambo yalianza kwenda mrama na mji huu kukosa umaarufu na nguvu kama hapo mwanzo. Mnamo karne ya 16 mji huu ulikuwa tayari chini ya utawla wa Wareno ambao walimiliki kila kitu kwenye mji huu.

Katika historia inaonyesha kuwa baada ya miaka 200 baadaye mji huu wa mji huu ulikuwa kwa kasi kubwa sana na kuwa maarufu zaidi kutona na bishara za watumwa ambazo kwa kiasi kikubwa zilifanywa na waarabu.

# TEMBO:
# Mhandisi wa mifumo ya kiikolojia?



NA MWANDISHI MAALUM

**HUYU ni mnyama aina ya tembo ambaye kwa historia fupi ndiye mnyama mkubwa kuliko wote ambao wanaishi nchi kavu. Kuna aina tatu za Tembo ambazo ni Tembo wa Asia, Tembo wa msituni (African forest elephant) na Tembo wa Nyika au Vichakani (African Bush elephant).**

Aina hii ya tatu ya Tembo ndio kubwa kuliko nyingine na jina lake la kisayansi ni Loxodonta Africana. Tembo hawa hupatikana katika nchi zilizo Kusini mwa Jangwa la Sahara ikiwemo Tanzania na wanaurefu wa pata futi 8 mpaka 13, anauzito wa wastani Kilo2500 mpaka 7000 na wana uwezo wa kuishi hadi miaka 70.

**CHAKULA**

Kwa siku Tembo anauwezo wa kula kilo zisizo pungua 136 ambazo zina mchanganyiko wa mizizi, majani,magome ya miti na matunda.,

**KUZALIANA**

Vilevile jike hubeba mimba kwa muda wa miezi 22 na kuzaa ndama mwenye kilo yapata 120 kilogramu.

Uongozi

Kama ilivyo kawada ya maisha ya viumbe hai mbalimbali, ikiwemo binadamu katika sualazima la uongozi, vile vile familia ya Tembo huongozwa na huongozwa na Tembo Jike ambaye ni mkubwa kiumbo na umri . Miongoni mwa kazi za tembo huyu kiongozi ni pamoja na kuliongoza kundi katika kutafuta chakula maji, n.k wakati wote wa maisha yao. Vile vile huyu ndio kiongozi wa misafara misafara ya tembo kutoka sehemu moja kwenda nyingine ambayo hupita katika shoroba mbalimbali.

**MHANDISI WA MFUMO WA IKOLOJIA**

Tembo hutumia meno yake mawili yaliyotokeza nje ya mdomo kuchimba kwenye mito iliyokauka ili kupata maji ambayo huwanufaisha wao pamoja na wanyama wengine.

Kinyesi cha Tembo ni chakula kwa wanyama wa aina mbaimbali kama vile jamii ya nyani na ndege. Mende Miwa (dung beetle)

Kinyesi cha tembo mara nyingi huwa na mchanganyiko wa mbegu za aina mbalimbali ambazo huweza kuota sehemu ambayo amejisaidia na hivyo kusaidia kusambaza au kuotesha mimea ambayo haikuwepo eneo hilo.

Tembo hung'oa miti kwa ajili ya chakula ambayo vile vile husaidia wanyama wengine kama Pundamilia ambao hupenda kula kwenye mazingira ya wazi.

Wanyama hawa husaidia kufungua njia kwa kuangusha vichaka na hivyo kuwafanya wanyama wengine wapiti kwa urahsi.

Mahali ambapo Tembo hukanyaga huacha alama za miguu mithili ya mashimo ambayo huwahifadhi viumbe wadogo kama chura ,haswa wakati wa mvua kwa kuyatumia mashimo hayo kwa kujisitiri na wkati mwingine kuzaliana. .

Vifaa ambavyo Mhandisi Tembo hutumia

**MKONGA**

Tembo hutumia kiungo hiki katika kupiga kelele ambazo huashiria mambo mbalimbali kama vile salamu, kufarijiana kama ilivyo mkono kwa binadamu, Kunusa, kupumua,kushikia vitu haswa chakula, kuchota maji ya kunywa na kuogea! Mhandisi Tembo huoga maji,vumbi au matope ikiwa na lengo la kujipoza na kujikinga na miale Mikali ya jua.

**MENO**

Haya ni meno mawili ambayo hayaachi kukua na hutumika katika kuchimba maji wakati wa kiangazi, kumegua magome ya miti kama mbuyu, kupigana hususani kwa tembo dume katika kipindi cha kuzaliana

**HITIMISHO**

Tembo ni miongoni mwa viumbe walio mbioni kutoweka kutokana na Ujangili na kukosekana kwa makazi yao ambayo yamesababishwa na binadamu kufana shughuli zao za maendelea kama vile mashamba, barabara, nyumba na mengineyo.



# MJUE ISHA:
## Mnyama anayejua kujilinda dhidi ya maadui

NA MWANDISHI MAALUM

**HUU ni mfululizo wa makala za wanyamapori ambazo nimekuwa nikikuletea mara kwa mara ili uweze kujua sifa, tabia, uhifadhi na uelekeo wa wanyama hawa hapa duniani hasa tukiangalizia hapa nchini kwetu Tanzania.**

Kuna faida kubwa sana tuzizpatazo kutokana na uwepo wa wanyama hawa hawa nchini na hasa pato la taifa kutokana na shughuli za kitalii zinazo liingizia taifa fedha nyingi za kigeni.

Basi nikusihi uendelee kuwa nami mwanzo mpaka mwisho wa makala hii ili uweze kujua katika makala ya leo tunamzu ngumzia mnyama gani na ana sifa gani.

Nina uhakika mara tu utakapokuwa umeisoma makala haya mwanzo mpaka mwisho tena kwa ufasaha basi utakuwa umepata kitu kipya tena chenye faida kubwa kuhusu utambuzi wa mnyma ambae ataibeba makala hii ya leo.

Kama kawaida bado tunaendelea na mfululizo wa kuwaelezea wanyama jamii ya swala kwani kundi hili lina wanyama aina mbali mbali sana ambao kadri tunavopata wasaa tutazidi kujulishana mpaka hapo tutakapo fikia ukomo wa wanyama hawa hususani kwa ambao wanapatikana hapa nchini kwetu Tanzania.

Katika makala haya tutamzungumzia swala ajulikanae kwa jina la 'Isha' ambaye kwa lugha ya Kiingereza anaitwa 'Steenbok'.

**MFAHAMU**

Isha ni mnyama apatikanaye kwenye kundi la wanyama jamii ya swala kama nilivokwisha dokeza hapo juu ambae anapatikana



maeneo ya mashariki na kusini barani Afrika hususani hapa nchini.

Mnyama huyu usipokuwa makini unaeza kumchanganya na mnyama Taya kwani wanafanana sana. Lakini kupitia makala haya naamini utaweza kuwatofautisha wanyama hawa ambao wanachanganya sana katika kuwatofautisha.

Isha ni miongoni mwa swala wenye umbo dogo kama walivo kina taya. Miili yao ina manyoa mafupi yenye rangi ya dhahabu inayoendana na kahawia au wakati mwingine manyoa yao huonekana kuwa na rangi ya wekundu.

Sehemu za mashavu, baadhi ya maeneo shingoni na kwa upande wa chini yaani kifuani mpaka tumboni wanyama hawa wana manyoa yenye rangi nyeupe.

Macho ya Isha ukiwaangalia vizuri utaona yamezungukwa na manyoa yenye rangi nyeupe na wana uwezo mkubwa sana wa kuona.

Wana masikio yaliyo chongoka ambayo sehemu za ndani za masikio yao yamezungukwa na alama nyeusi za mistari yenye umbo kama kidole. Hawa ni miongoni mwa wanyama wenye uwezo mkubwa sana wa kusikia. Kwa pamoja madume na majike wana matezi yenye rangi nyeuusi ambayo yanaonekana sehemu ya mbele ya macho yao. Wana kwato ngumu zilizo chongoka ambazo huwasaidia kuchimba vyakula vyenye asili ya mizizi. Wanyama hawa wana miguu mirefu na iliyo nyooka zaidi.

Madume pekee ndo huwa na pembe ambazo zimenyooka, ziko sambamba, nyororo na zilizo chongoka. Pembe hizi hurefuka na kufikia urefu wa sentimita 7 hadi 19.

Isha ni wanyama ambao wanafanya shughuli zao majira ya asubuhi na mchana, na maranyingi kipindi cha joto kali hupendelea kupumzika kwenye kivuli chini ya miti.

Hupenda kujisaidia kwenye mashimo na kisha kuyafukia mashimo hayo. Hii huwasaidia wanyama hawa wasigundulike kirahisi maeneo waliyopo hasa kutokana na maadui zao.

Wanapohisi kuna adui wanyama hawa hutulia na kujificha lakini adui anapowakaribia hukimbia na kutafuta maficho mengine hasa kwenye mashimo yaliyo achwa na wanyama kama mhanga.

Dume na jike huishi mbalimbali na hukutana kipindi wanapotaka kuzaliana tu hivyo dume mmoja huwa na jike mmoja tu na eneo lao huwa na ukubwa wa hekari 4 mpaka 100.

Tofauti na swala walio wengi, isha hawatumii matezi kuweka mipaka katika maeneo yao na maranyingi hutumia kinyesi tu au kuwafukuza Isha wengine ambao wameingia kwenye eneo lao.

Isha mkubwa hufikia urefu wa sentimita 70 hadi 95. Kimo cha isha hufikia sentimita 45 hadi 60. Wanyama hawa huwa na uzito wa kilogramu 7 hadi 16.

**MAZINGIRA**

Kama nilitangulia kusema hapo juu, wanyama hawa wanapatikana Afrika mashariki na kusini mwa Afrika tu na si kwingine kokote kule duniani. Wanapedelea mazingira yenye majani tu na tafiti zinaonesha kuwa wanyama hawa ni kwa nadra sana kuwaona katika maeneo ambayo kwa asilimia kubwa ardhi imetawaliwa na miti.



# DRAKE MDOGO TU KWA LAMAR

LOS ANGELES, Marekani

**LILE bifu kati ya marapa Kendrick Lamar na Drake lilinogeshwa na hafla ya tuzo za Grammy wikiendi iliyopita. Ni baada ya Lamar kumpiku Drake kwa kubeba tuzo.**

Lamar, kupitia wimbo 'aliom-dis' Drake uitwao 'Not Like Us', alinyakua tuzo tano, ikiwamo ile ya Wimbo Bora wa Hip hop.


## TEMS ALA FAGIO LA DAVIDO

LAGOS, Nigeria

**SUPASTAA wa Lagos, Davido, ameibuka na kumpongeza bibiye anayefanya vizuri katika soko la muziki wa Nigeria, Tems.**

Katika hafla ya Grammy iliyofanyika Jumapili ya wiki iliyopita, Tems aliibeba tuzo ya Msanii Bora wa Mwaka wa Afrika.

Tems aliibeba tuzo hiyo kupitia ngoma yake ya 'Love Me Jeje', akiwapiku mastaa kibao, wakiwamo Yemi Alade na Wizkid.




## JAY-Z NOMA TUPU

LOS ANGELES, Marekani

**RAPA wa viwango vya juu, Jay-Z, ameandika historia ya kuwa msanii mwenye tuzo nyingi katika historia ya Grammy.**

Wikiendi iliyopita, supastaa huyo mwenye mkwanja wa kutosha alibeba tuzo yake ya 25 katika hafla ya msimu wa 47 wa Grammy.

Kwa kufanya hivyo, sasa Jay-Z anakuwa amemzidi tuzo moja mshikaji wake, Kanye West, ambaye ana 24.





## MATHYS TEL AITAKA UNITED

MANCHESTER, England

**MSHAMBULIAJI wa kimataifa wa Ufaransa, Mathys Tel, amemwambia wakala wake kuwa anaitaka Manchester United.**

Mazungumzo kati ya Man United na klabu yake ya Bayern Munich yamekwama, hivyo inasubiriwa kiangazi, mwaka huu.

## SPURS YAMTAKA KROUPI

LONDON, England

**TOTTENHAM inaangalia uwezekano wa kuinasa saini ya mpachikaji mabao wa kimataifa wa Ufaransa, Eli Junior Kroupi.**

Kwa mujibu wa ripoti, Tottenham inatoana jasho na klabu za Chelsea na West Ham United katika dili hilo.



# PAULOVIC KUIBUKIA PALACE

LONDON, England

**KLABU ya Crystal Palace iko kwenye mawindo ya kuinasa saini ya beki wa kati wa AC Milan, Strahinja Pavlovic.**


Kwa mujibu wa ripoti, kocha wa Palace, Oliver Glasner, ndiye anayeshinikiza usajili wa mchezaji huyo.

## FLAMENGO, JORGINHO KUMALIZANA

LONDON, England

**KIUNGO wa kimataifa wa Italia, Jorginho, huenda akamalizana na mabosi wa klabu ya Flamengo ya Brazil.**

Kwa mujibu wa ripoti, Jorginho mwenye umri wa miaka 33, atatua Brazil mwishoni mwa msimu huu.



## TZIMAS ANAWANIWA BRIGHTON

LONDON, England

**KLABU ya Brighton inampigia hesabu mshambuliaji wa kimataifa wa Ugiriki anayekipiga PAOK, Stefanos Tzimas.**

Kwa sasa, nyota huyo mwenye umri wa miaka 19 anakipiga kwa mkopo katika klabu ya Nurnberg.



BUSATI
MICHEZO
Alhamisi Februari 6, 2025 Tovuti: www.tanzaniabora.



# MILOUD: YANGA NAJUA MNACHOTAKA

## NI KOCHA MPYA ALIYEBABA MIKOBA YA RAMOVIC, AKUTANA NA WACHEZAJI

NA ELLY SARONGO

**KOCHA Miloud Hamdi ambaye amechukua mikoba rasmi ya kuifundisha Yanga toka kwa Sead Ramavic aliyeondoka, amepiga mkwara mzito na kusema 'anajua alichofuata Tanzania'.**

Miloud ambaye amewasili jijini Dar es Salaam jana, alikutana na wachezaji na kuwaambia wazi nini kile anachokitaka kwao, huku akitabanaisha wazi kwake hakuna staa ila kile unachofanya uwanjani ndicho kitakachokugeuza uwe staa kwake.

"Miloud ametua jana na tayari amekutana na wachezaji wote na kuwaambia matarajio yao kwake, hana mzaha katika hili na amewataka wahakikishe wanaipambania nembo ya Yanga kwa nguvu zote.

"Amezungumza nao kifupi, amewaambia atakutana na mchezaji mmoja mmoja ili kuzungumza naye, ili ajue changamoto ya kila mmoja na amewataka wafunguke kwake," kilisema chanzo chetu.

Miloud mzaliwa wa Algeria mwenye uraia wa Ufaransa, anakuja Yanga kuchukua nafasi ya Ramovic ambaye ameondoka katika kikosi hicho kwa kile kinachodaiwa kupata dili mpya sehemu nyingine.

Juzi, Ramovic aliwashtua wachezaji akiwaaga rasmi kwamba baada ya mchezo dhidi ya KenGold uliopigwa jana hataendelea kuwa kocha wa timu hiyo.

"Ni kweli kocha ametuaga baada ya mazoezi kumalizika, kwakweli imetushtua sana, kwanza tulidhani labda amegombana na uongozi lakini ameweka wazi kwamba amepata nafasi ya kwenda kufanya kazi sehemu nyingine," kilipasha chazo chetu.

# Simba 'kuwajua wabaya wao'




NA MWANDISHI WETU

**SHIRIKISHO la Soka Barani Afrika (CAF) limetangaza tarehe ya droo ya robo fainali ya mashindano ya Klabu Bingwa na Kombe la Shirikisho Afrika kwa timu zilizofuzu hatua hiyo msimu huu ambapo pia limepanga tukio hilo kufanyika Doha, Qatar Februari 20.**

Baada ya kumaliza katika nafasi ya kwanza kwenye Kundi A, la Kombe la Shirikisho Afrika, Simba inatarajia kukutana na timu mojawapo iliyomaliza katika nafasi ya pili kwenye kundi lake ambapo inaweza kukutana na ama Asec Mimosas (Ivory Coast), Stellenbosch (Afrika kusin) na Al Masry (Misri).

Simba ambao ndiyo wawakilishi pekee wa Tanzania katika michuano ya Kimataifa walifanikiwa kufuzu hatua ya robo fainali baada ya kumaliza nafasi ya kwanza katika kundi A ambapo ilikuwa imepangwa na timu za CS Constantine, CS Sfaxien na Bravos do Maquis ya Angola.